

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SELIKARI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

SHULE YA SEKONDARI LUPIRO
S.L.P 288 ,
MAHENGE/ULANGA.

13/12/2020

KUMBA NA; LPSS/ADSM/INST/2020.

JINA LA MWANAFUNZI

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPIRO KIDATO CHA KWANZA 2020

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Lupiro kidato cha kwanza kwa mwaka 2020. Nachukua nafasi hii kukupongeza kupata bahati hii, ambayo wachache huipata. Ni matumaini yangu utaitumia vizuri nafasi hii uliyopewa kwa manufaa yako binafsi, familia na taifa kwa ujumla. Hivyo usiichezee hata kidogo.

Shule ipo katika kijiji cha Mbasa, kata ya Lupiro, Tarafa ya Lupiro, wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro. Ufikapo lupiro mjini elekea njia iendayo Malinyi umbali wa kilometra moja na nusu. Masomo yataanza 11/01/2020 siku ya jumatatu, unatakiwa ufile shulen i siku hiyo, ukichelelwa kufika utaipoteza nafasi hiyo. Ufikapo shulen onana na mkuu wa shule au makamu kwa ajili ya usajili. Pia hakikisha umepitia hospitalini upate vipimo kutoka kwa daktari na kuijaza fomu iliyombatanishwa na barua hii. Pia hakikisha umesoma sheria na kanuni na kuzielewa vizuri.

MAHITAJI MUHIMU

A. SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

- Mashati mapya meupe mawili mikono mifupi aina ya tomato. Usitumie shati ulilotumia shule ya msingi.
- Suluari mpya mbili kijani kibichi zeny marinda (Jani la mgomba) **upana wa chini size 16 hadi 20,yenye turn up,usishone suluari kwa staili ya modal.**
- Viatu vya ngozi na vya kamba vyenye soli fupi siyo buti.
- Soksi nyeusi zisizo na mistari wala rangi nyingine.
- Mkanda wa ngozi wenye kichuma shikizi (bunkle ya heshima)
- Fulana (T-shirt) na tai vinapatikana hapa shulen.

B. SARE KWA WASICHANA

- Mashati mapya meupe mawili mikono mifupi aina ya tomato. Usitumie shati ulilotumia shule ya msingi.
- Sketi mbili za kijani kibichi (Jani la mgomba) urefu wa sketi **iguse kiatu** pia vazi la juba na nusu kazu nyeupe kwa waislamu, (mtandio au juba ya rangi nyingine yeoyote hairuhusiwi)
- Viatu vya kamba vyeusi vyenye soli fupi.
- Fulana (T-shirt) na tai vinapatikana hapa shulen.

NB: MZAZI / MLEZI ATAKAYEPATA CHANGAMOTO YA RANGI YA KITAMBAA SAHIHI AFIKE SHULENI MAPEMA ATAONESHWA KITAMBA HICHO .

C. VIFAA VINGINE

(I) ZANA ZA KAZI NA USAFI

- Kila mwanafunzi atakayekuja kuripoti anatakiwa kuja na ufagio, faili Aidha ndoo, jembe na panga ataagizwa kuja navyo kwa ajili ya usafi na kazi zingine na kurudi navyo nyumbani.

➤

(II) VIFAA VYA MASOMO

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na begi la kuwekea madaftari, madaftari makubwa Counter Book Quire 3, yasiyopungua 11, kalamu za wino na mkaa pamoja na mkebe (mathematical set) 1 na dictionary.

(III) VIFAA VYA MICHEZO

Kila mwanafunzi anatakiwa awe na vifaa vya michezo, bukta ya bluu kwa wavulana na tshirt ya bluu pamoja na raba za michezo. Wasichana awe na tracksuit ya bluu na tshirt ya bluu na raba za michezo.

SHERIA ZA JUMLA

1. Heshima kwa walimu wote. Viongozi, wazazi, wanafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni jambo la lazima.
3. Kuwahi kufika katika kila shughuli za shule na zinginezo utakazopewa.
4. Kutimiza usafi wa mwili wako, mavazi yako na mazingira ya shule.
5. Kuvaa sare rasmi za shule wakati wote utakapokuwepo shulenii
6. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
7. Kuheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa taifa na kutii kengele ni sualaa la lazima.
8. Msichana harusiwi kusuka nywele.
9. Mvulana haruhusiwi kufuga ndevu.

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE BILA ONYO

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile; uvutaji wa bangi, cocaine heroine, mirungi, kubeli, sigara.
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba au kusababisha mimba
10. Kutoa mimba, kuharibu mimba au kusaidia utoaji wa mimba.
11. Kugoma, kuchochea au kuongoza na kuvuruga amani usalama wa shule na watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi uwapo shulenii
14. Kucheza kamali ya aina yeyote ile na pool table.
15. Kuhunduria kumbi za starehe, kukutwa nyumba za kulala wageni bila ruhusa maalumu
16. Utoro sugu.

ASANTE,



EDWINI E. MOLLEL

MKUU WA SHULE

0689825037

MKUU WA SHULE
LUPIRO SEKONDARI
S.I. P 288
MAHENGE TULI